

TARGETER WINGS
KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI
GREDI 3 - 2021



Wings
006

SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina

Jinsia:

Mvulana

Msichana

Jina la shule

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

	Swali la 1	Swali la 2	Swali la 3	Swali la 4
Idadi ya alama	15	5	20	10
Alama sahihi				

1. KUSOMA KWA SAUTI

Soma maneno haya kwa sauti (Alama 15)

- | | | | |
|---------------|-----------------|---------------|-------------|
| 1. Bendera | 2. Kifyekeo | 3. Dharau | 4. Mbung'o |
| 5. Kiranja | 6. Mayowe | 7. Mazingira | 8. Daktari |
| 9. Palilia | 10. Tarakilishi | 11. Kuvunjika | 12. Daftari |
| 13. Mkokoteni | 14. Mnunuzi | 15. Mwewe | |

2. UFAHAMU

1. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata. (alama 5)

Likizo iliyopita tulienda na mama kwa halati. Halati yangu anaishi mbali sana. Tulisimama kwenye kituo cha basi tukingoja basi. Basi lilifika, tukaingia na safari ya mjini ikaanza.

Basi hilo liliendeshwa kwa kasi mno. Abiria waliteta sana. Niliona gari moshi likipita kwenye reli. Sokoni kulikuwa na pikipiki. Malori yalibeba mboga na mahindi. Shangazi alikuwa ametungoja. Alitubeba kwa gari lake.

1. Shangazi aliishi wapi? _____

2. Tulitumia chombo gani kusafiri? _____

3. Kwa nini abiria ndani ya basi waliteta? _____

4. Kuendesha gari kwa kasi ni kuendesha gari vipi? _____

5. Andika kichwa cha hadithi hii _____

3. SARUFI (Alama 20)

1. Andika vinyume vya vitenzi hivi (alama 5)

- (a) Anika _____
- (b) Tia _____
- (c) Meza _____
- (d) Lia _____
- (e) Washa _____

2. Andika kwa maneno au nambari (alama 5)

- (a) 306 _____
- (b) Mia mbili _____
- (c) 55 _____
- (d) Themanini _____
- (e) Mia tano na kumi _____

3. Chagua kimilikishi sahihi kujaza pengo (alama 5)

(vyao, chake, yake, lake, wako)

- (a) Mama _____ alimpeleka hospitalini.
- (b) Jino _____ linauma.
- (c) Mlango _____ umevunjika.
- (d) Vitambaa _____ vimeraruka.
- (e) Kijana wa kijiji _____ alipata zawadi.

4. Andika wingi wa sentensi hizi. (alama 5)

- (a) Kitabu hiki kimeraruka _____
- (b) Wewe unafaa nguo _____
- (c) Daktari anatibu mgonjwa _____
- (d) Ua hili linapendeza _____
- (e) Kalamu imepotea _____

4. KUANDIKA (Alama 10)

Andika sentensi tano kuhusu.

RAFIKI YANGU

Jumla (alama 50)